JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI

SHULE YA SEKONDARI IDETEMA

S L P 15

MGOLOLO

0/12/2020

KUMB.ED/IDSS/VOL.1/11

NDUGU_____

_____

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IDETEMA SS WILAYA YA MUFINDI MKOA WA IRINGA MWAKA 2021

1.0 _ UTANGULIZI

Ninayo furaha kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021 na unatakiwa kuripoti tar 11/01/2021 siku ya Jumatatu saa 1:30 asubuhi. Shule ya sekondari Idetema ipo wilaya ya Mufindi tarafa ya Kasanga kata ya Idete

Shule ni ya kutwa na ni ya mchanganyiko wa wanafunzi wavulana na wasichana kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne. Masomo yanayofundishwa ni :- Uraia, Kiswahili, Kiingereza, Jiografia, Historia, Fizikia, Bailojia, Hisabati, na literature kwa kidato cha tatu na cha nne

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

SARE ZA SHULE

A. WAVULANA

- Suruali ya rangi ya kijani jeshi (02) na bluu bahari (02)
- Mashati meupe mawili ya mikono mirefu
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kisigino kifupi vya kufunga na kamba jozi mbili (02)
- Soksi nyeupe pea mbili (02)
- Bukta na fulana za michezo zenye rangi ya ya Taifa
- Raba za michezo
- Tai moja rangi ya kijani jeshi na bluu bahari
- Sweta la bluu lenye mshono wa V shingoni lisilo na maandishi

A. WASICHANA

- Sketi rangi ya kijani jeshi mbili (02) na bluu bahari mbili (02) ziwe ndefu sana
- Blauzi nyeupe mbili mikono mirefu
- Viatu vyeusi jozi mbili vya kufunga na kamba. Skuna na viatu vyenye visigino virefu havitakiwi
- Soksi nyeupe jozi mbili
- Sweta la bluu mshono wa V kifuani lisilo na maandishi

- Bukta na fulana za michezo zenye rangi ya taifa
- Tai moja rangi ya kijani jeshi na bluu bahari
- Suruali ya kijani jeshi (02) na bluu bahari (02)

NB: Kwa wale watakaovaa hijabu ni lazima rangi ya hijabu ifanane na rangi ya sare ya shule mfano kuwa nyeupe kama blauzi

MAHITAJI MENGINE YA SHULE

- Madaftari makubwa 18 ya masomo 9 darasani 9 kwa ajili ya mazoezi na majaribio ya kila wiki. Kila somo litakuwa na daftari lake maalumu la mazoezi na majaribio
- Begi (hand bag) dogo jeusi kwa ajili ya kuwekea daftari na vifaa vingine vya masomo
- Kamusi (dictionary) ya kiingereza – Kiswahili au kiingereza – kiingereza
- Mkebe wa hesabu mmoja (mathematic set 1)
- Rimu moja ya karatasi kwa ajili ya matumizi binafsi ya mwanafunzi
- Jembe 1, fyekeo 1 kindoo na cheleo kwa ajili ya shughuli za usafi binafsi kwa mwanafunzi

NB: ukaguzi wa sare utafanyika ili kuhakikisha kila mwanafunzi ana sare na vifaa alivyoa agizwa

3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria na. 10 ya mwaka 1996. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi yenye dhamana na na elimu nchini na ofisi ya Raisi – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yamefafanuliwa kwa maandishi katika Appendix A,B na C

KARIBU SANA IDETEMA SEKONDARI

…….

DEULE P.M

MKUU WA SHULE

APPENDIX B

JINA LA MWANAFUNZI …… SAHIHI …….

SHULE YA SEKONDARI IDETEMA

S L P 15 MGOLOLO – IRINGA

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE AMBAZO MWANAFUNZI ANATAKIWA KUZIFUATA

A. SHERIA

1. Mwanafunzi anatakiwa kusimama na kumsalimia mwalimu au mtu yeyote aliye mzidi umri anapopita,anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano
2. Mwanafunzi haruhusiwi kutumia lugha mbaya popote,wakati wowote na kwa mtu yeyote
3. Mwanafunzi anatakiwa kuwaheshimu wafanyakazi wote walioko shuleni kama walezi wake
4. Mwanafunzi anatakiwa kushirikiana na kusaidiana na wenzake katika kazi na masomo
5. Mwanafunzi anatakiwa kuthamini na kuheshimu kazi za aina zote
6. Mwanafunzi HARUHUSIWI kufanya mambo yafuatayo
    1. Kuvuta sigara,bangi
    2. Kutumia madawa ya kulevya
    3. Kufuga kucha wala kuwa na nywele zisizo na utaratibu
    4. Kupaka rangi kwenye kucha au midomoni
    5. Kufuga ndevu
    6. Kuvaa mavazi yasiyokuwa na heshima
    7. Kugombana
    8. Kuchelewa

B. MAHUDHURIO

i. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa

ii. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria kazi zote za mikono

iii. Mwanafunzi anatakiwa kufanya mambo yafuatayo:-
    a) Kuandika notes zote
    b) Kufanya mazoezi yote anayopewa na mwalimu
    c) Kutunza madaftari yake vizuri

iv. Mwanafunzi anatakiwa kujali muda uliopangwa, yaani KUWAHI SHULENI KWENYE VIPINDI DARASANI

v. Mwanafunzi anatakiwa kuwahi kwenye shughuli zote

vi. Mwanafunzi anatakiwa kukimbia mara asikiapo wito wa kengele au anapoitwa na mwalimu, au mtu yeyote anayemzidi umri

C. **UVAAJI WA SARE ZA SHULE**

i. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa katika sare ya shule wakati wote awapo shuleni

ii. Anatakiwa kuvaa sare wakati wa:-
    a) Masomo darasani
    b) Anapotoka nje ya shule kwa shughuli za kishule
    c) Mhadhara wa shule
    d) Anapokwenda hospitali
    e) Kwenye maandamano

iii. Anatakiwa kuhakikisha kuwa sare yake ni safi wakati wote

D. **MIPAKA**

i. Mwanafunzi asitoke nje ya mipaka ya shule bila kibali maalum

ii. Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo:-

a) Vilabu vya pombe
b) Baa
c) Nyumba za kulala wageni
d) Majumba ya starehe
e) Nyumba za walimu zisiwe na mazoea kwa mwanafunzi, epuka!

E. MAKOSA AMBAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga
3. Ulevi/uvutaji wa bangi/madawa ya kulevya
4. Makosa ya jinai
5. Kupiga /kupigana
6. Kuharibu mali ya umma
7. Kudharau bendera
8. Kuoa au kuolewa
9. Kupata mimba au kusababisha mimba
10. Kutoa mimba au kusababisha kutoa mimba
11. Kupanga mikutano ya kuvuruga amani shuleni
12. Kugoma adhabu kwa makusudi
13. Matusi kwa kauli au maandishi,lugha ya dharau,makelele,ugomvi ni marufuku
14. Uzinzi,urafiki wa kimapenzi,ubakaji,unyanyasi wa kijinsia,utoro,kiburi ni marufuku
15. Kuwa na simu ya mkononi

…….

DEULE P.M

APPENDIX C

SHULE YA SEKONDARI IDETEMA
S L P 15 MGOLOLO

DAKTARI ……
HOSPITALI ……
S L P ……

FOMU YA KUPIMWA AFYA MWANAFUNZI

Tafadhali tunaomba umpime mwanafunzi aliyetajwa hapo juu kwa gharama za mzazi wake, na uthibitishe kama ataweza kumudu masomo ya sekondari shule hii. Ni muhimu apimwe kabla ya kuja hapa

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI IDETEMA
S L P 15
MGOLOLO

YAH: MWANAFUNZI .

Matokeo ya vipimo vya afya ya mwanafunzi aliyetajwa hapo juu

1. Urine …….
2. Stool …….
3. BP ……..
4. Pregnancy test ……
5. Chest …….
6. Physical abnormality ……..

Nathibitisha kuwa mwanafunzi huyu …….. ataweza/hataweza kumudu masomo ya sekondari kwa sababu

……
……

JINA LA DAKTARI SAHIHI/CHEO TAREHE

…….. …… ……..